

Tarehe:

KUH: Ombi la Usaidizi kwa “Mtoto Asiye na Makao” kulingana na Sheria ya McKinney-Vento

Anwani ya mahali ambapo mtoto anaishi kwa sasa:

Anwani ya mahali ambapo mtoto alikuwa anaishi kabla ya “kuwa bila makao”:

Shule unayotaka:

Mwalimu Mkuu wa shule ya mtoto:

Jina la mtoto, Tarehe ya Kuzaliwa, Darasa:

Mpendwa _____ (mwalimu mkuu):

_____ (jina la mtoto) “hana/hawana makao” chini ya Sheria ya McKinney-Vento na wanalindwa na masharti yake. **(Chagua moja:)**

	Mtoto anaweza kusomea shule hii kwa sababu alikuwa anasomea hapa mbeleni (“shule aliyokuwa akisomea”).
	Mtoto anaweza kusomea shule hii kwa sababu iko karibu na makao yake ya sasa.

Sihitaji kuomba nafasi ya kujiandikisha shuleni kwa kuzingatia eneo ninaloishi, wala kuleta stakabadhi kamili za kujiandikisha kama vile ithibati ya makao. Pia, naomba nisaidiwe kwa: **(chagua zaidi ya moja)**

	IEP		Mpango wa 504
	Kiamshakinywa na chakula cha mchana cha shule		Sare za timu ya spoti
	Sare za shule		Kutolipa ada ya Klabu au ya Timu ya Spoti
	Usafiri		Nakala za taarifa za shule na chanjo za hapo awali
	Bidhaa za kutumiwa shuleni		Usaidizi wa kupanga miadi ya matibabu au matibabu ya meno
	Kutolipa karo		Nguo na viatu vya somo la michezo/mazoezi ya mwili
	Usaidizi wa kutuma ombi la kujiunga na chuo kikuu		Kutolipa ada ya mtihani wa SAT au ACT
	Usaidizi wa mtoto kujifunza lugha ya Kiingereza		Mwingine:

Ikiwa una maswali au matatizo yoyote, tafadhali wasiliana nami. Unaweza kuwasiliana nami kupitia _____. Asante kwa ushirikiano wako.

Wako mwaminifu,

Jina la Mzazi:

Barua hii ya Sheria ya McKinney Vento iliwasilishwa na mimi, mzazi/mlezi, kwa

_____ mnamo _____.

Jina la Mfanyakazi wa Shule Aliyeipokea

Tarehe

Maagizo ya Kuandika Barua ya Kuomba Usaidizi kwa ajili ya Mtoto “Asiye na Makao”

1. Andika tarehe ambayo unamaliza kuandika na kutia saini barua
2. Andika anwani ya mahali ambapo mtoto anaishi kwa sasa na anwani ya mahali ambapo mtoto alikuwa akiishi hapo awali
3. Andika jina la shule ambayo unataka mtoto asomee na jina la Mwalimu Mkuu
4. Andika jina la mtoto wako, tarehe yake ya kuzaliwa, na darasa
5. Andika jina la Mwalimu Mkuu
6. Chagua MOJA kati ya visanduku hivi viwili, na uweke alama ya usahihi au x
7. Weka alama ya usahihi au x karibu na visanduku vingi kama unavyohitaji.
8. Andika namba yako ya simu au anwani ya barua pepe au zote mbili.
9. Weka saini kisha uandike jina lako
10. Wasilisha barua, wewe mwenyewe, kupitia barua pepe, sanduku la posta, au kwa faksi. Ukiwasilisha barua wewe mwenyewe, andika jina la aliyeipokea barua hiyo pamoja na tarehe ambayo ulimpokeza.
11. **JAMBO MUHIMU SANA:** Hifadhi nakala ya barua hiyo
 - a. Unaweza kuipiga picha barua hiyo kwa kutumia simu yako kisha ujitumie kupitia barua pepe. Kujitumia kwa barua pepe kutasaidia iwapo simu itapotea, iharibike, au picha hiyo ikifutika.
 - b. Unaweza kuhifadhi nakala ya karatasi katika faili zako.

*Advocates for Basic Legal Equality, Inc. na Legal Aid of Western Ohio, Inc. (ABLE) ni mashirika ya kisheria yasiyo ya faida yanayoshughulikia mahitaji ya kisheria ya kiraia ya watu binafsi na familia zilizo na mapato madogo katika magharibi mwa Ohio. Habari hizi si ushauri wa kisheria. Ni habari za kawaida. Habari hizi hazitumiki kama mbadala wa kuzungumza na wakili kuhusu hali yako. Huenda bado ukahitaji usaidizi kutoka kwa wakili. *Ilisishwa kwa mara ya mwisho Novemba 19, 2019*